

## MASWALI MACHACHE YA USANIFISHAJI WA KISWAHILI (JINGINE AU LINGINE?)

NELLY V. GROMOVA

---

This article discusses one particular issue of Swahili standardization. Which is, in *Kiswahili Sanifu*, the correct concordial agreement to be applied to the lexeme *-ingine* ('other')? Should it be treated like an adjective, as 'classical' works in Swahili grammar claim as well as current educational books do? How can efforts in favour of standardization comply with the appearance of different variants of concordial agreement?

---

### 1. Utangulizi

Kila mwalimu anayeshughulika na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni mara kwa mara hukabiliwa na maswali ambayo hayajibiki kwa urahisi. Swali mojawapo lihusulo sarufi ya Kiswahili ni swali juu ya upatanisho wa kisarufi wa kivumishi *-ingine*.

Mpaka siku hizi watumiaji wa lugha ya Kiswahili hawajakubaliana, matumizi gani ni sahihi yaani lazima kutumia viambishi-patanishi vilivyo sawa na viambishi awali vya nomino (ling. *ji cho jeusi jingine*, *nyumba nyeusi nyingine*) ama viambishi-patanishi tofauti (ling. *ji cho jeusi lingine*, *nyumba nyeusi zingine*).

Makala hii inazungumzia matumizi ya kivumishi hiki katika maandishi na maongezi ikijaribu kuangalia sababu za kiisimu za matumizi ya aina mbili tofauti.

Swali hilo ni mojawapo kati ya maswali mengine mazito ya usanifishaji wa Kiswahili ambao “ni jambo la dharura iwapo lugha hii itakua na kutekeleza majukumu muhimu katika enzi hii ya utandawazi” (Choge 2006: 29). Wataalamu wengi walioshiriki kwenye Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI mwaka 2005 walijadili kwa kina vipengele vya sarufi ya Kiswahili sanifu na matumizi yake kwenye jamii.

### 2. Umbo gani ni sahihi?

Karibu wanasarufi wote walioandika vitabu vyao vya sarufi ya Kiswahili wakieleza upatanishi kati ya nomino na vivumishi wanataja mzizi *-ingine* unaopatanishwa na nomino kufuatana na kanuni za kipatanisho cha vivumishi. Hao ni wanasarufi walio wengi ambao ni wageni na Waswahili kuanzia Ashton (1944) hadi watungaji wa *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA 2001).

Lakini kuna wanasarufi na watumiaji wa lugha ya Kiswahili wasio wachache ambao wanapendelea kutumia mzizi unaotofautiana kidogo. Kwa mfano, mtungaji wa kitabu kitiwacho *Mazoezi na marudio ya Gateway KCPE. Kiswahili*, Wallah bin Wallah (1997) akijaribu “kuainisha matumizi halisi na fasaha ya baadhi ya vivumishi vinavyokanganya” anasema juu

ya mzizi *-ngine* (ibid.: XIV, 20). Mwandishi mashuhuri Said A. Mohamed anapendelea kutumia mzizi *-engine*, mathalan katika riwaya yake *Babu Alipofufuka* (2001) unaweza kusoma *mtu mwengine, jambo jengine, kazi nyengine* (tz. ibid.: passim). Ashton alitilia mkazo kwamba upatanishi wa kivumishi hiki kama ule “*chengine and vyengine are used in Mombasa*” (Ashton 1944: 47) maana yake hayo ni matumizi si ya Kiswahili Sanifu bali ni ya mojawapo ya lahaja za Kiswahili.

Tukiwafundisha wanafunzi Kiswahili Sanifu inatupasa tusijali matumizi niliyoyataja juu? Lakini Wallah bin Wallah ni mmojawapo wa waalimu wenye tajriba kubwa ya utunzaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani katika kiwango cha darasa la nane katika shule za msingi huko Kenya. Na Said A. Mohamed ni mwandishi mashuhuri wa Kiswahili ambaye tunawapendekeza wanafunzi wetu wasome vitabu vyake. Hivyo linazuka swali la kwanza: mzizi gani ni sahihi? Mzizi *-ngine* peke yake? Au wanafunzi na wasomaji wawe huru katika matumizi yao? Ikiwa tunakubali na maoni hayo, hatuwezi kusema juu ya lugha sanifu.

### 3. Upatanisho gani ni sahihi?

#### 3.1. Kanuni mbili za upatanisho wa kisarufi

Wanasarufi wote wanakubali kwamba mzizi huo *-ngine* ni wa kivumishi. Basi ukiwa kivumishi, mzizi huo hauna budi kupatanishwa kisarufi na nomino sawa na vivumishi vingine halisi. Ikumbukwe kuwa lugha ya Kiswahili ina makundi mawili ya viambishi awali:

(a) la kwanza ni kundi la viambishi awali vya nomino na vya vivumishi, ambavyo kwa kiasi kikubwa havitofautini kimaumbo, vinaandamana na viambishi vya umbo nomino, kwa mfano *mtu mrefu, miti mirefu*;

b) kundi la pili ni viambishi patanishi ambavyo vinaundwa kutokana na viambishi awali vya nomino, lakini vinaambatanishwa kwenye mashina ya kitenzi au kiwakilishi kwa kanuni maalum za kimofolojia-kifonetiki. Kwenye safu hii ya upatanishi wa kisarufi Kiswahili hakitumii konsonanti nazali [m/n] (isipokuwa katika ngeli ya mahali mu-), kwa mfano kiambishi awali wa nomino ya ngeli ya 3 yaani *mu-* kikidondosha [m] kinabadilika kiwe *u-*, kiambishi awali cha ngeli ya 9, ambacho umbo lake la ndani katika mamebantu lilikuwa *in-*, kinapoteza ile nazali [n] kikawa kiambishi patanishi *i-*, sawa na kiambishi awali cha ngeli ya 10 *zin-* zikawa *zi-* (viambishi awali *in-* na *zin-* vinapatikana kwa mfano latoka lugha ya kipogoro: *zintaata* ‘ajabu’, *zimpula* ‘pua’). Tena konsonanti [j] ya kiambishi awali cha ngeli ya 5 hubadilika kiwe [l].

Hivyo, sarufi ya Kiswahili sanifu inadai uwiano sahihi wa kimofolojia-kifonetiki baina ya kiambishi awali cha nomino na viambishi patanishi vya kisarufi vya vivumishi na viwakilishi kama ufuatao: *jua jeupe jingine letu, nyumba nyeupe nyingine zetu*, na kadhalika.

ngeli	kiambishi awali cha nomino	kiambishi patanishi cha kivumishi	kiambishi patanishi cha kiwakilishi na kitenzi
1	mu-/m-/mw-	mw-/m-	yu-/a-/w-
2	wa-/w-	wa-/w-	wa-
3	mu-/m-/mw-	m-/mw	u-

## USANIFISHAJI WA KISWAHILI

ngeli	kiambishi awali cha nomino	kiambishi patanishi cha kivumishi	kiambishi patanishi cha kiwakilishi na kitenzi
4	mi-	mi-/my-	i-
5	ji-/j-/Ø	ji-/j-/Ø	li-
6	ma-/m-	ma-/m-	ya-
7	ki-/ch-	ki-/ch-	ki-/ch-
8	vi-/vy-	vi-/vy-	vi-/vy-
9	n-/m-/ny-/Ø	n-/m-/ny-/Ø	i-
10	n-/m-/ny-/Ø	n-/m-/ny-/Ø	zi-
11	u-	m-/mw-	u-
15	ku-/kw-	ku-/kw-	ku-
16	pa-	pa-/p-	pa-
17	(ku-/kw-)	ku-/kw-	ku-
18	(mu-/mw-)	mu-/mw-	mu-/m-

### 3.2. Mkanganyo wa kanuni za upatanisho

Lakini mara nyingi unaweza kusoma au kusikia matumizi ya aina tofauti ya upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano, katika riwaya ya Edwin Sembaza iitwayo *Funke Bugebuge* (1999) iliyowahi kushinda tuzo la kwanza katika mashindano ya uandishi wa Afrika Mashariki yali-yodhaminiwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili utapata mifano kama hii: *kazi zingine* (ibid.: 1), *nyakati zingine* (ibid.: 89), *neni lingine* (ibid.: 101), ingawa mara nyingine unaweza kuona upatanishi kama *wakati mwingine*, *aina nyingine*, na kadhalika.

Katika magazeti ya Kiswahili na vyombo vingine vya habari ambavyo huthaminiwa na kusomwa na wengi kila siku, matumizi ya aina hiyo yanapatikana kwa wingi. Kwa mfano, katika gazeti la kiserikali *Uhuru* utasoma: “Sikukuu hiyo imekuwa ikiwahusisha pia watu wa dini *zingine*”; “kiongozi kafuja mali ya umma sehemu moja na kutokana na kosa hilo kuhamishwa sehemu au eneo *lingine*”; “Watanзания washughulika na biashara *ingine*”.

Hiyo ina maana kwamba watumiaji wa Kiswahili wanakanganya aina mbili za upatanishi wa kisarufi yaani upatanishi wa kivumishi na upatanishi wa kiwakilishi. Mara kwa mara wataalam wa Kiswahili wanawatahadharisha watu wasifanye makosa ya aina hiyo. Kwa mfano Wallah bin Wallah anasisitiza kuwa “kitabu chake kinatubainisha kwamba usahihi wa vivumishi *-ngine* ni; *swali jingine* si *lingine*, *maswali mengine* si *mingine*, *nguo (umoja) nyingine* si *ingine*, *nguo (wingi) nyingine* si *zingine*” (Wallah 1997: XIV).

Kuna sababu gani ya mkanganyo kama huo? Ni lahaja za Kiswahili zinazoathiri Kiswahili sanifu? Au lugha sanifu inaathiriwa na matamshi ya watumiaji wa Kiswahili ambao lugha zao za mama si za Kibantu ama lugha nyenzie za Kibantu lakini tofauti na Kiswahili fasaha? Inafahamika kwamba watanzia wengi wanazo athari za mwingiliano wa lugha za kikabila katika Kiswahili. Na hapo ni muhimu kuhifadhi usahihi wa Kiswahili sanifu.

### 3.3. Sababu za kiisimu za mkanganyo

Tukiangalia kwa makini mifano iliyotolewa hapo juu tunaweza kuona wazi kwamba matumizi yasiyo sahihi hutokea kwa kiasi kikubwa sio katika ngeli zote 18, bali katika ngeli ya 5 na 9/10 yaani katika ngeli tatu tu za *ji-li* na *n-i/n-zi*. Kwa jumla hutumika mzizi *-ingine*. Utata unaojitokeza katika matumizi ya kiambishi patanishi cha ngeli ya 10 ungeweza kufanunuliwa namna hii: ukisema *nyumba nyingine* huwezi kutambua neno hili ni la umoja au wingi. Pengine hiyo ndiyo sababu, watu wanaposema *twende katika hospitali zingine* wanajaribu kubainisha wingi wa neno.

Kuhusu matumizi ya kivumishi chenye umbo *lingine* sina maelezo tosha. Inawezekana kwamba *jambo jingine* linalowafanya wazungumzaji wa Kiswahili kupatanisha kivumishi – *ingine* kama kiwakilishi ni athari ya kisintaksia. Kama kawaida kivumishi *-ingine* kinasimama mwishoni mwa tungo-kirai ya nomino baada ya kiwakilishi. Inawezekana kufikiria tu kwamba viambishi patanishi vya kiwakilishi vinaathiri kiambishi patanishi cha kivumishi kama vile *hospitali zetu > zingine*.

### 4. Usanifishaji wa lugha ni jambo la lazima?

Lugha katika maisha yake hubadilikabadilika na kupitia hatua mbalimbali. Mabadiliko ya kimsamiati na ya kisarufi pia ni mambo ya kuweka maanani hasa kwa walimu na wanafunzi. Wataalamu wa lugha hujaribu kukisanifisha Kiswahili na kukisahihisha, kwa sababu

[u]kuaji wa lugha kwa kasi kubwa namna hiyo unahitaji mwongozo wa vitabu vya rejea vya kuaminika na vinavyokidhi mahitaji ya wakati uliopo, kuanzia kamusi, vitabu vya sarufi, na vitabu vingine vya matumizi bora. La sivyo, mwalimu wa Kiswahili mashuleni anapotea njia na kupotosha wanafunzi wake, ambao ndilo taifa la kesho, na mwandishi wa Kiswahili anakuwa mbabaishaji anayedhuru nchi nzima kwa maandishi yake, badala ya kuboresha lugha na kuendeleza fasihi yake (Ruhumbika 2006: 225).

Ikumbukwe miaka ya themanini ya karne iliyopita ambapo wataalamu wa lugha walieleza magazetini na redioni makosa yanayofanywa mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili. Inawezekana kusema kwamba kiwango kipya cha usanifishaji wa sarufi na msamiati wa Kiswahili kimefikiliwa baada ya TUKI ilipotolea SAMAKISA (2001) na toleo la pili la *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS 2004). Baada ya hapo watumiaji wa Kiswahili, wanazuoni kwa wazungumzaji wa kawaida, waalimu kwa wanafunzi, waandishi wa vitabu kwa waandishi wa magazeti, walipata msaada mkubwa.

Lakini, kwa upande mwingine, sote tunajua kuwa lugha si kitu kilichoganda, lugha inaendelea na kukua bila ya kusita. Kile kilichoelezwa kama kosa, kinaweza kuwa sahihi bada ya muda kupita. Kwa mfano, matumizi ya neno *mkupuo* kuwa na maana ya hatua, yalielezwa kama tafsiri isiyo sahihi ya neno la Kiingereza *phase* (Idarus 1983: 178). Lakini katika Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili (TUKI 1996) neno *phase* linatafsiriwa kama *awamu* au *mkupuo* (uk. 569).

## USANIFISHAJI WA KISWAHILI

### 5. Hitimisho

Kusema kweli, hakuna hatari kubwa, watu wanapokanganya matumizi ya viambishi patanishi. Dhamira yao ya kufahamiana na kuwasiliana inaweza kutekelezwa kwa kutojali makosa fulani ya kisarufi. Lakini wataalam wa lugha na waandishi wanaofikiria usafi na ufasaha wa Kiswahili, hawana budi waangalie matumizi sahihi ya Kiswahili, hasa katika maandishi yao, kwa sababu athari zao ndizo kubwa sana kwenye lugha. Wasomaji, ambao wengi wao hawana kisomo cha kutosha, wanachukulia lugha ya maandishi kama lugha sahihi, sanifu na yenye ufasaha. Kuhifadhi, kulinda na kuitetea usafi wa lugha kama nguzo ya utamaduni wa Kiswahili ni jukumu la waandishi na wataalamu wa lugha.

Kwa upande mwingine, mpaka leo bado hakuna taasisi moja ambayo ingedai kanuni sahihi za Kiswahili sanifu zitumiwe wa watumiaji wote wa Kiswahili hasa mashuleni. Kwa hivyo hatuwezi kubashiri maendeleo ya baadaye ya lugha. Hatujajua mwelekeo gani utashinda, yaani juhudi za wataalamu wa lugha pamoja na wote wengine wanaopenda kutumia Kiswahili sanifu, ama matumizi ya wazungumzaji wa kawaida ambao wengi wao wanamudu lugha mbili au zaidi, na Kiswahili si lugha yao ya kwanza? Si ajabu kwamba baada ya makumi ya miaka tutaona kuwa maneno *lingine* na *zingine* yatatambuliwa kama maneno sahihi kisarufi. Historia ya lugha yoyote ile inaonyesha kwamba ushindi upo kwenye upande wa wazungumzaji wa kawaida wa lugha walio wengi zaidi. Waswahili wasema “mtoto umleavyo ndivyo akuavyo”. Atakuaje mtoto huyo?

### Marejeo

Ashton, Ethel O. 1944. *Swahili Grammar (Including Intonation)*. London: Longmans.

Choge, Susan Chebet. 2006. Kusanifisha Kiswahili Sanifu: Hitaji katika karne ya 21. S. S. Sewangi & J. S. Madumulla (Eds.). *Makala ya Kongamano la Kimatifa la Jubilei ya TUKI 2005* 1. Dar es Salaam: TUKI. uk. 25-35.

Idarus, A. S. 1983. Makosa yanayofanywa mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili. TUKI (Ed.). *Lugha ya Kiswahili (Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1)*. Dar es Salaam: TUKI. uk. 173-187.

Kihore, Yared M., David P. B. Massamba & Yohana P. Msanjila. 2001. *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA)*. Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, Said Ahmed. 2001. *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ruhumbika, Gabriel. 2006. Mwandishi wa Kiswahili na Lugha yake katika Tanzania Huru. *Makala ya Kongamano la Kimatifa la Jubilei ya TUKI 2005* 2. Dar es Salaam: TUKI. uk. 225-232.

Senzaba, Edwin. 1999. *Funke Bugebuge*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

TUKI. 1996. *English – Swahili Dictionary. Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

NELLY V. GROMOVA

TUKI. 2004. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili*. Dar es Salaam et al.: Oxford University Press & TUKI.

*Uhuru*. Gazeti la kila siku. Matoleo mbalimbali yasiyotajwa.

Wallah bin Wallah. 1997. *Mazoezi na Marudio ya Gateway KCPE Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.